

NANI ANAWEZA

KUNISAIDIA ?

AHUKO PEKE YAKO; HUDUMA ZIFUATAZO ZINAWEZA KUKUSAIDIYA:

Ili **KUSIKILIZWA**, kupata **MAELEZO**, **MWONGOZO** (kupata malazi, huduma za kisheria, usaidizi wa kijamii au kisaikolojia, ...)

0800 30 030 (masaa 24/24 kila siku, bila malipo na bila kujulikana) au **ongee** kwa ujumbe kwenye anuani

www.ecouteviolencesconjugales.be

UKIWA HATARINI. Pigia simu **polisi** kwa namba 101 au lombaa **msaada** kwa namba **112**

Écoute Violences Conjugales


0800 30 030

24/7 + GRATUIT + ANONYME

www.ecouteviolencesconjugales.be

MHAMIAJI NA MWATHIRIWA WA UJEURI KATIKA NDOA AU KATIKA FAMILIA

JE, NI ZIPI HAKI ZANGU?



ULIKUJA UBELJII KUJIUNGA NA MEMBA WA FAMILIA ZAKO NA UNAISHI HALI YA UJEURI NYUMBANI?

Écoute Violences Conjugales

0800 30 030

24/7 + GRATUIT + ANONYME



Wallonie



Kipeperushi hiki kimebuniwa kutoka kwenye brosha ya «Mhamiaji na mwathiriwa wa Ujeuri wa nyumbani, ni zipi haki zangu», iliyotayarishwa na "CIRES" na jukwaa husiani la Brussels "ESPER".

NI NINI UJEURI KATIKA NDOA AU FAMILIA ?

UJEURI KATIKA NDOA AU FAMILIA INAWEZA KUWA :

UTAWALA

tishio ya kunyanganywa makaratasi vya Sheria, ao kukurudisha inchini yako



KIFEDHA

kuacha mtu bila pesa, bila chakula, bila mashini ya kuleta joto



KIMWILI

kupigwa, kusukumwa, Kumnyonga kwa kitazi



UJINSIA

kulazimu au kulazimisha mwingiliano wa kingono kwa nguvu



MANENO

kutukana, kutishia



KISAIKOLOJIA

kutishia, kutia kizuizini, kuzuia mtu kusoma au ku fanya kazi, kufedhehesha na kudhalilisha



WEWE NA WATOTO WAKO MNA MA HAKI

Mna haki ya **kuishi bila ujeuri**. Ujeuri ndani ya ndoa au katika familia ni hatia chini ya sheria za Ubeljiji.



Mna haki ya **kuongea na watu walio karibu na nyinyi ambao wanaweza kuwasaidia na kuwaongoza**: familia yako, daktari wako, OFISI ya Uzazi na Utoto (ONE), shule ya watoto...



Pia una haki ya **kuitisha usaidizi na kuripoti kwa polisi**.



Hata kama cheti chako cha ukaazi kinategemea wewe kuishi na mume wako, mke wako au familia yako, una haki ya **kutoka nyumbani**.



Ulizia na hifadhi ithibati ushahidi wa ujeuri : vyeti vya kimatibabu, ripoti za polisi, ushahidi, picha, baruapepe, SMS, rekodi...

Ili kudumisha **cheti chako cha ukaazi**, ni lazima ukidhi mahitaji fulani. Wakili au watoa huduma zilizofanywa maalum wanaweza kukusaidia.

